

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke)

Simu I: +255 22-2928132
Faks: +255 22-2928137
Barua pepe : temeke@temekemc.go.tz
Tovuti: <http://www.temekemc.go.tz>



Ofisi ya Mkurugenzi,
92 Barabara ya Mandela/Taifa
S.L.P 46343,
15883 -DAR ES SALAAM,

Tarehe: 07, AGOSTI, 2017

ZABUNI NA. LGA/016/2017-18/HQ/NC/Preq 02 (MARUDIO)

KWA AJILI YA

UNUNUZI WA HUDUMA YA UZOAJI WA TAKA NGUMU KUTOKA KWENYE KATA MBALIMBALI NDANI YA MANISPAA YA TEMEKE KUPELEKA KWENYE DAMPO LA PUGU KINYAMWEZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

1. Halmashauri ya Manispaa ya Temeke katika kuboresha huduma ya uzoaji wa taka, imebinafisha kazi ya **UZOAJI WA TAKA NGUMU KUTOKA KWENYE KATA MBALIMBALI NDANI YA MANISPAA YA TEMEKE NA KUPELEKA KWENYE DAMPO LA PUGU KINYAMWEZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018** kwa kuwatumia wazabuni ambao wataingia Mkataba na Manispaa kuendesha shughuli hizo.
2. Halmashauri ya Manispaa ya Temeke sasa inatangaza zabuni ya **uzoaji wa taka kutoka kwenye kata mbalimbali ndani ya manispaa ya Temeke kwenda kwenye dampo la Pugu Kinyamwezi** kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 kwa kata zifuatazo:-
Azimio, Buza, Chamazi, Keko, Kilakala, Kilungule, Kurasini, Makangarawe, Mianzini, Miburani, Sandali na Toangoma.
NB: Mzabuni haruhusiwi kuomba zaidi ya kata moja
3. Halmashauri inakaribisha maombi kutoka kwa Vikundi/Taasisi/Makampuni yenye uwezo na uzoefu wa kufanya shughuli hizo za uzoaji wa taka ngumu katika kata tajwa hapo (2) juu.
4. Masharti na maelekezo ya zabuni.
 - i. Kikundi/Taasisi/Kampuni itakayoomba zabuni iwe imesajiliwa kisheria.
 - ii. **Ada ya maombi ni sh 50,000.00 kwa kablasha moja la zabuni.** Malipo yatafanyika kwa fedha taslim na kupokelewa na karani wa fedha katika ofisi ya Mweka Hazina wa Manispaa ya Temeke na kukatiwa stakabadhi.

- iii. Dhamana ya zabuni: Dhamana ya zabuni (Bid Securing declaration)
- iv. Maombi yote yatatumia nyaraka za zabuni zinazopatikana kwenye ofisi ya *Katibu wa bodi ya zabuni Manispaa ya Temeke* baada ya kulipia ada ya maombi.
- v. Maombi yote ya zabuni yawe na nakala halisi (original) na nakala vivuli (copy) mbili (2) zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa: **"ZABUNI NA. LGA/016/2017-18/HQ/NC/Preq.02 (MARUDIO); KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA YA UZOAJI WA TAKA KUTOKA KWENYE KATA YA.....(Taja jina la kata mzabuni anayoomba) NDANI YA MANISPAA YA TEMEKE KWENDA KWENYE DAMPO LA PUGU KINYAMWEZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018"** Pamoja na anuani ifuatayo:

**Katibu wa Bodi ya Zabuni,
Halmashauri ya Manispaa Temeke,
S L P 46343,
Dar es salaam.**

Maombi yawasilishwe kwenye ofisi Na. 2 ya Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi na Ugavi katika Manispaa ya Temeke iliyopo barabara ya Mandela/Taifa Dar es Salaam

- 5. Mwisho wa kutuma maombi ni siku ya **JUMATATU, 21 AGOSTI, 2017** kabla au saa 5.00 asubuhi na ufunguzi utafanyika mara baada ya muda wa kupokelewa kuisha mbele ya watoa huduma au wawakilishi wa watoa huduma waliochagua kuhudhuria ufunguzi kwenye ukumbi wa mikutano wa PMU uliopo makao makuu ya manispaa ya Temeke.
- 6. Maombi yote ambayo yatatumwa baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha kupita hayatafanyiwa kazi.

**Mkurugenzi
MANISPAA YA TEMEKE**